## JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

## BUNGE LA TANZANIA

## KAMATI YA BUNGE YA BAJETI

# MAONI YA KAMATI KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA MFUKO WA MAHAKAMA KWA MWAKA WA FEDHA 2016/17 PAMOJA NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2017/18

OFISI YA BUNGE
**DODOMA**

**25 APRILI, 2017**

## MAONI YA KAMATI KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA MFUKO WA MAHAKAMA KWA MWAKA WA FEDHA 2016/17 PAMOJA NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2017/18

### 1.0 UTANGULIZI.

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa kanuni ya 99(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2016, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bajeti, kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Mfuko wa Mahakama kwa Mwaka wa Fedha 2016/17 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha wa 2017/18.

**Mheshimiwa Spika,** kamati ilikutana na Waziri wa Fedha na Mipango, Waziri wa Katiba na Sheria pamoja na Mtendaji Mkuu wa Mahakama na kujadiliana na kufanya mashauriano kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Mfuko wa Mahakama kwa Mwaka wa Fedha 2016/17 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha wa 2017/18. Mashauriano haya yamefanyika kwa mujibu wa kifungu cha 75 cha Sheria ya Bajeti Na. 11 ya Mwaka 2015.

### 2.0 UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA MFUKO WA MAHAKAMA KWA MWAKA 2016/17

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa Katiba, jukumu kubwa la Mahakama ni kusimamia utoaji wa haki. Katika kutekeleza hili Mahakama imefanikiwa kutekeleza yafuatayo:-

a) Mahakama imefanikiwa kuanzisha divisheni Maalum ya Mahakama Kuu inayoshughulikia makosa ya rushwa na uhujumu uchumi;

b) Watumishi 539 wamepata mafunzo ya muda mfupi ya ndani ya nchi, baadhi yao ni Waheshimiwa Majaji 57, Wasajili 3, Naibu Wasajili 9 na Mahakimu 144;

c) Imekarabati Mahakama Kuu Dar es Salaam, Tanga na Ukarabati wa Mahakama kuu ya Mbeya upo katika hatua za mwisho;

d) Imesambaza nakala mbalimbali za Vitabu vya mwongozo wa usimamizi na ukaguzi wa shughuli za Mahakama ili kuwezesha Mahakama nchini kutoa huduma bora zaidi kwa wananchi;

e) Imeendelea kukamilisha miradi yake ya maendeleo ikiwemo ujenzi na ukarabati wa majengo ya Mahakama kwa gharama nafuu katika maeneo ya Kibaha, Bagamoyo, Kigamboni, Mkuranga, Kawe na Kinyerezi;

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na utekelezaji wa majukumu haya, bado Mfuko wa Mahakama unakabiliwa na changamoto mbalimbali kama vile:-

I. Utolewaji wa fedha na usioendana na Mpango Kazi wa Mfuko wa Mahakama;

II. Uhaba wa watumishi wenye sifa zinazotakiwa kwenya kada mbalimbali;

III. Bajeti ndogo ya Mfuko wa Mahakama isiyolingana na mahitaji halisi.

## 3.0. MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI YA MWAKA WA FEDHA 2016/2017

**Mheshimiwa Spika**, Katika mwaka wa fedha 2016/17 Mfuko wa Mahakama – **Fungu 40** uliidhinishiwa jumla ya kiasi cha **Sh.131,627,043,504** Kati ya fedha hizo **Sh.50,345,775,000** ni kwa ajili ya Mishahara (PE), **Sh.34,519,534,000** kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC), na **Sh.46,761,734,504** kwa ajili ya Mpango wa Maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha mwezi Julai 2016 hadi Februari 2017 jumla ya **shilingi 55,427,630,446.56** zilitolewa na Wizara ya Fedha kwa **Fungu 40** kwa ajili ya mishahara na matumizi mengineyo, hii ikiwa sawa na **asilimia 42** ya fedha zilizotengwa kwa mwaka 2016/17. Aidha, kwa upande wa fedha za maendeleo jumla ya **shilingi 829,593,993** zilitolewa hii ikiwa sawa na **asilimia 2** ya bajeti iliyotengwa kwa mwaka 2016/17 (**shilingi 46,561,734,000**).

**Mheshimiwa Spika,** Hata hivyo pamoja na kupokea fedha hizi bado kumeonekana kuna changamoto kubwa ya kutokutolewa fedha kwa wakati kwa fungu husika na hivyo kuathiri utekelezaji wa baadhi ya majukumu ya Mfuko wa Mahakama. Aidha, Kamati ya Bajeti ilifanya mashauriano na Serikali na kukubaliana kiasi cha fedha kilichobakia kwenye fungu hili kitolewe kabla ya tarehe 30 Juni 2017.

## 4.0 MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA MFUKO WA MAHAKAMA KWA MWAKA WA FEDHA 2017/18.

**Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka wa Fedha 2017/18, fedha zilizokasimiwa kwenye Mfuko wa Mahakama zimetengwa katika maeneo mbalimbali kwa ajili ya kuhakikisha Mahakama inatekeleza majukumu yake ya Kikatiba. Baadhi ya majukumu ambayo yamepangwa kutekelezwa katika bajeti ya mwaka 2017/18 ni kama yafuatayo:

a) kuendelea kutoa hukumu ya haki sawa kwa wote na kwa wakati;

b) kuimarisha uongozi, utawala bora na uwajibikaji kwa Mahakama pamoja na kuongeza upatikanaji wa haraka wa huduma za Mahakama kwa wananchi;

c) kuimarisha ufanisi katika kazi za Mahakama kwa kutumia TEHAMA;

d) Kuongeza mahusiano baina ya wadau wa nje na ndani ya Mahakama;

e) kujenga taswira mpya ya Mahakama yenye mtazamo chanya;

## 4.1 Maduhuli

**Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka wa fedha 2017/18 Mfuko wa Mahakama umepanga kukusanya maduhuli ya kiasi cha **Sh. 9,318,061,200** ikilinganishwa na makadirio ya **shilingi 6,504,132,435** mwaka 2016/17.

## 4.2 Matumizi ya Kawaida na Maendeleo

**Mheshimiwa Spika**, Katika mwaka wa fedha 2017/18 Mfuko wa Mahakama umetengewa jumla ya **Sh.125,117,029,000;** baada ya Serikali kushauriana na Kamati ya Bajeti na kuongezea fedha za matumizi mengineyo (OC) kwa mfuko huu kiasi cha **shilingi 6,000,000,000.**

**Mheshimiwa Spika**, Kati ya fedha hizo zilizotengwa; **Sh.56,477,636,000** ni kwa ajili ya Mishahara, **Sh.50,481,382,000** ni kwa ajili ya Matumizi ya Mengineyo *(OC)* na **Sh.18,158,011,000** ni kwa ajili ya maendeleo ambapo kati ya kiasi hicho **Sh.17,000,000,000** ni fedha za ndani na **Sh.1,158,011,000** ni fedha za nje. Mchanganuo wa namna fedha za Matumizi ya Kawaida na maendeleo zitakavyotumika zimeanishwa kwenye jedwali lifuatalo.

**JEDWALI : Mchanganuo wa Makisio ya Bajeti kwa mwaka 2017/18**

| **NA.** | **MAELEZO** | **BAJETI YA MWAKA 2016/2017** | **MAKISIO YA MWAKA 2017/2018** |
|---|---|---|---|
| 1. | Mishahara | 50,345,775,000 | 56,477,636,000 |
| 2 | Matumizi Mengineyo (OC) | 34,519,534,000 | 50,481,382,000 |
| 3 | **Matumizi Ya Maendeleo** | **46,761,734,504** | **18,158,011,000** |
| | Fedha za Ndani | 24,000,000,000 | 17,000,000,000 |
| | Fedha za Nje | 22,761,734,504 | 1,158,011,000 |
| 4 | **Jumla ya Matumizi ya Kawaida na Maendeleo** | **131,627,043,504** | **125,117,029,000** |

## 5.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

5.1 **Kwa kuwa**, Tathmini ya utekelezaji wa Bajeti ya Mfuko wa Mahakama kwa mwaka wa fedha 2016/2017 inaonyesha kuwa hadi kufikia mwezi Machi 2017; mfuko huu unakabiliwa na changamoto ya kutopokea fedha kwa wakati pamoja na kupokea fedha pungufu tofauti na ilivyoombwa na hivyo kuathiri utekelezaji wa majukumu ya Mfuko huu hasa kwa upande wa miradi ya maendeleo'

**Hivyo basi,** Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kwamba kwa mwaka wa fedha wa 2017/2018 Mfuko wa Mahakama unapatiwa fedha kwa wakati na kwa mujibu wa maelekezo ya Sheria ya Bajeti (2015) kama zilivyoidhinishwa na Bunge.

5.2 **Kwa kuwa**, Mfuko wa Mahakama unakabiliwa na uhaba wa watumishi wenye sifa zinazotakiwa katika kada mbalimbali,

**Hivyo basi**, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha inaongeza idadi ya watumishi wanaohitajika kwenye kada mbalimbali kwa awamu ili kusaidia kutekeleza majukumu ya Mfuko huu;

5.3 **Kwa kuwa**, mtiririko wa utoaji fedha kwenye Mfuko wa Mahakama umekuwa hauzingatii Mpango Kazi wa Mfuko husika,

**Hivyo basi**, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha inazingatia maelekezo ya kifungu cha 48 cha Sheria ya Bajeti Na. 11 ya mwaka 2015 kinachoitaka Hazina kutoa fedha kwenda Mfuko wa Mahakama kwa kila robo mwaka. Pia, Serikali ihakikishe ukomo unaotolewa unazingatia hali halisi ya mahitaji ya Mahakama,

5.4 **Kwa kuwa**, bajeti iliyotolewa kwa mwaka 2016/17 haikidhi mahitaji ya msingi ya Mfuko wa Mahakama hadi kupelekea Mfuko huu kukabiliwa na madeni mbalimbali yanayohusu posho ya wazee wa baraza, malipo ya pango la nyumba za kuishi Majaji, ofisi za kuendesha Mahakama pamoja na madai mbalimbali ya watumishi,

**Hivyo basi**, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha inamalizia kupeleka kwenye Mfuko wa Mahakama bakaa ya matumizi mengineyo kiasi cha **shilingi bilioni 20** katika bajeti ya mwaka 2016/17 ili Mfuko huu uweze kulipa baadhi ya madeni hayo

## 6.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika,** naomba nihitimishe kwa kukushukuru wewe Mheshimiwa Spika na Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson (Mb), Naibu Spika kwa kuongoza vema mashauriano kati ya Kamati ya Bajeti na Serikali. Namshukuru Mheshimiwa Dkt. Philip Mpango (Mb), Waziri wa Fedha na Mipango na Mheshimiwa Dkt Ashatu Kijaji (Mb), Naibu Waziri wa Fedha na Mipango kwa ushirikiano wao kwa Kamati. Aidha, Kamati inamshukuru pia Mheshimiwa Proff. Palamagamba Kabudi , (Mb), Waziri wa Katiba na Sheria na Mtendaji Mkuu wa Mahakama kwa kushirikiana na Kamati wakati wa majadiliano.

**Mheshimiwa Spika,** napenda kuwashukuru wajumbe wa Kamati hii kwa umakini wao katika kujadili na kutoa maoni na mapendekezo mbalimbali kuhusu Bajeti ya Mfuko wa Mahakama. Naomba kuwatambua wajumbe hao kama ifuatavyo;

1) Mhe. Hawa Abdulrahman Ghasia, Mb – Mwenyekiti
2) Mhe. Josephat Sinkamba Kandege, Mb - M/ Mwenyekiti
3) Mhe. Hamida Mohamedi Abdallah, Mb

4) Mhe. David Ernest Silinde, Mb

5) Mhe. Mbaraka Kitwana Dau, Mb

6) Mhe. Mendrad Lutengano Kigola, Mb

7) Mhe. Maria Ndilla Kangoye, Mb

8) Mhe. Susan Peter Maselle, Mb

9) Mhe. Agustino Manyanda Masele, Mb

10) Mhe. Freeman AikaelMbowe, Mb

11) Mhe. Flatei Gregory Massay, Mb

12) Mhe. Makame Kassim Makame, Mb

13) Mhe. Janet ZebedayoMbene, Mb

14) Mhe. Cecil David Mwambe, Mb

15) Mhe. Susana Chogisasi Mgonukulima, Mb

16) Mhe. Subira Khamis Mgalu, Mb

17) Mhe. Juma Hamad Omar, Mb

18) Mhe. Ali Hassan Omari, Mb

19) Mhe. Martha Jachi Umbulla, Mb

20) Mhe. Jerome Bwanausi, Mb

21) Mhe. Jitu Vrajlal Soni, Mb

22) Mhe. Abdallah M.  Bulembo, Mb

23) Mhe. Andrew John Chenge, Mb

24) Mhe. Mussa A. Zungu, Mb

25) Mhe. Japhet Ngalilonga Hasunga, Mb

26) Mhe. Dalali Peter Kafumu, Mb

27) Mhe. Albert Obama Ntabaliba, Mb

**MheshimiwaSpika,** napenda kuchukua fursa hii, pia kumshukuru Katibu wa Bunge Dkt Thomas Kashililah kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake ipasavyo, pamoja na Sekretarieti ya Kamati ya Bajeti kwa kuipa ushauri wa kitaalamu Kamati hadi kukamilika kwa taarifa hii.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya maelezo hayo naliomba Bunge lako tukufu sasa lijadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Mfuko wa Mahakama – Fungu 40, kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 kama yalivyowasilishwa na Waziri wa Katiba na Sheria.

**Mheshimiwa Spika,** naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja hii.

Subira Khamis Mgalu, Mb

**Kny: MWENYEKITI**
**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI**

25 APRILI, 2017